**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 28 Februari, 2022**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mjumbe wa Kamati ya Wabunge watano wanaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:**

Ripoti ya Wabunge watano wanaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

105. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Katika kufikia makubaliano ya kupunguza kero za Muungano kati ya Serikali zote mbili za SMT na SMZ suala la ajira za taasisi za Muungano nalo lilipatiwa ufumbuzi kwamba zigawiwe asilimia 79 kwa upande wa Tanzania na asilimia 21% kwa upande wa Zanzibar, makubaliano hayo yalifikiwa zaidi ya miaka nane iliyopita.

(a) Kwa kuwa makubaliano hayo ni muhimu sana Je, ni hatua gani zimeshachukuliwa katika utekelezaji wa jambo hilo.

(b) Kwa kuwa kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) Zanzibar inakuwa sehemu ya Jamhuri ya Muungano na kwenye Jumuiya hiyo kuna mgawanyo wa nafasi za utumishi hasa zile za juu. Je, ni wazanzibari wangapi wanafanya kazi katika jumuiya hiyo kupitia dirisha la Tanzania.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

25. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Miongoni mwa juhudi zilizochukuliwa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kujenga miji yenye usafi wa hali ya juu na kuondoa adha ya maji taka katika maeneo mbali mbali ya wananchi, ni pamoja na kujenga mitaro ya maji taka, kupitia fedha za wafadhili na hata fedha za Serikali yenyewe. Hata hivyo, mitaro hiyo haikujengwa katika maeneo yote ya miji, ikiwemo eneo la Minazini, Chake Chake Pemba.

Je, ni lini Serikali itaujenga mtaro wa maji taka uliopo Minazini Pemba.

28. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Wananchi wa Zanzibar huwa wanasherehekea siku za Iddi kwa kufanya sherehe katika viwanja mbali mbali ambapo sherehe hizo husimamiwa na Manispaa, Baraza ya Mji na Halmashauri. Aidha wakati wa sherehe hizo baadhi ya wajasiriamali huwa wanauza bidhaa mbali mbali hata hivyo wajasiriamali hao wamekuwa wakilalamikia utaratibu wa utoaji wa maeneo ya kufanyia biashara hasa kwa Manispaa ya Mjini kwamba hucheleweshwa hadi mwezi 29 Ramadhan hali ambayo huwaletea usumbufu mkubwa.

(a) Kwa kuwa siku za sikukuu huwa zinajulikana mapema kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa kuwapatia maeneo hayo angalau siku tatu kabla ya kuanza kwa sherehe hizo.

(b) Yapo malalamiko kwamba pamoja na wajasiriamali hao kulipia fedha maeneo hayo, wapo watu wengine ambao hawalipii maeneo ya wazi bila ya kuchukuliwa hatua na Manispaa. Je, ni kwa nini wafanyabishara hao wanaachiwa kufanya biashara kinyume na utaratibu.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

6. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Naipongeza Serikali kwa kujenga majengo ya ofisi katika mji wetu wa Chake Chake, kwa lengo la kusogeza huduma hizo kwa wananchi wa Pemba. Hata hivyo, bado kuna usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaoishi maeneo ya mbali, wanapata shida ya kuzifuata huduma za Serikali katika majengo ya Chake Chake.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza kujenga majengo kama hayo ya Chake Chake katika miji mengine ya Pemba.

(b) Kwa nini Serikali haioni haja ya ofisi zake zilizopo Chake Chake zikahamia pamoja katika majengo hayo yaliyopo eneo la Gombani, ili kurahisisha huduma za kimaendeleo.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

70. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kwa kuwa wananchi wa shehia ya Mgogoni - Jimbo la Wawi hufuata huduma ya matibabu katika kituo cha afya Mvumoni, na kwa kuwa kituo hicho kipo mbali na makaazi ya wananchi wa jimbo hilo, jambo ambalo huwaletea usumbufu mkubwa katika kufuata huduma hiyo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea kituo cha afya wananchi wa shehia ya Mgogoni.

113. MHESHIMIWA HAMZA HASSAN JUMA (Jimbo la Shaurimoyo) Atamuuliza Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Hivi karibuni katika Hospital yetu ya Rufaa ya Mnazi Mmoja kumekuwa na ukosefu wa vyuma kwa ajili ya kuekewa wagonjwa ambao wamepata ajali, jambo ambalo wananchi wamekuwa wakisumbuka kupata matibabu kwa wakati ambapo mgonjwa akichelewa kupata tiba kwa wakati huweza kumletea tatizo jengine ikiwemo kukatwa viungo.

(a) Je, Mhe. Waziri suala hilo unataarifa nalo.

(b) Kama ndio, ukosefu huu umesababishwa na kitu gani.

(c) Je, ni sababu zipi zilizopelekea kuwepo kwa uhaba wa vifaa vya tiba (vyuma vya majeruhi wa ajali).

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

88. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa elimu ya juu ya Tanzania inajulikana kuanzia Elimu ya Chuo Kikuu, na kwa kuwa suala la elimu ya juu ni miongoni mwa mambo ya Muungano kwa mujibu wa Jadweli la Kwanza la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

(a) Je, ni sababu zipi zinazopelekea skuli za Tanzania Bara na skuli za Zanzibar kufanya pamoja mitihani ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita.

(b) Je, ni sababu zipi zinazopelekea wafanyakazi wa elimu ya juu Zanzibar kutokulipwa mishahara yao sawa na wafanyakazi wa elimu ya juu Tanzania Bara.

90. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Miundombinu bora na imara husaidia sana katika kuwawezesha wanafunzi kumudu na kufaulu vyema mitihani na masomo yao.

Je, Wizara ipo tayari kuzitembelea skuli za Mwanakwerekwe C, F, G, D na skuli ya Magogoni kwa lengo la kujionea hali halisi la uharibifu wa miundombinu, ili kwa pamoja tukishirikiana na viongozi wa jimbo kutafuta ufumbuzi wa haraka.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

15. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae): Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kupitia utekelezaji wa Ilani ya CCM 2020-2025 na ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kufufua michezo na kurudisha hamasa ya michezo Zanzibar.

(a) Kwa mwaka wa utekelezaji wa 2020-2021, ni michezo gani iliyofufuliwa hadi sasa.

(b) Katika harakati za ufufuaji wa michezo hiyo, kipaumbele cha Serikali ni katika ngazi gani.

20. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu ya nane inachukuwa jitihada kubwa kuimarisha michezo, lakini bado ligi kuu ya Zanzibar inakosa umaarufu.

(a) Je, ni hatua gani Serikali inazichukuwa kulisimamia Shirikisho la Mpira (ZFF) Zanzibar.

(b) Ni mikakati gani ZFF wanaichukuwa kuisimamia ligi kuu ya Zanzibar ili ivutie kama zamani.

(c) Je, Changamoto zilizopo kwa sasa na zinazoathiri ligi kuu ni lini zitatafutiwa ufumbuzi.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

59. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika vijiji vya Kilindi, Chanjaani Mji Mpya, Nungwi na Kigunda ziliombwa nguzo 24 za umeme tangu mwaka 2018 na mpaka sasa wananchi wa vijiji hivyo bado hawajapatiwa nguzo hizo.

Je, ni lini Serikali itawapatia huduma hii wananchi wa vijiji hivi.

156. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Wananchi wa jimbo la Pandani wanaipongeza Serikali na Rais Mwinyi kufuatia maelekezo mapya kuhusu kuunganishwa umeme mijini na vijijini na mahitaji ya nguzo za umeme. Hata hivyo, katika maeneo ya Mwane kuna vijiji vya Miburani, Ndige na Jitenge ambapo umeme umepitishwa barabarani tu.

(a) Je, ni lini Serikali itaanza kuusambaza umeme katika vijiji vya Miburani, Ndige na Jitenge.

(b) Je, ni upi utaratibu mpya wa upatikanaji wa nguzo za kuvuta umeme kutoka barabarani na kuupeleka katika vijiji hivyo.

(c) Je, ni yepi majukumu ya Serikali na majukumu ya wananchi husika katika kusambaza umeme kutoka barabarani na kuupeleka umeme huo vijijini.

**<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

39. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Wananchi wa visiwa vya Zanzibar wameendelea kupongeza juhudi za Serikali kwa uboreshaji wa safari za anga, jambo linaloleta ufanisi na kurahisisha harakati za kimaisha. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko juu ya baadhi ya mashirika yanayotoa huduma hizo kutokujali muda kwa upande wa wasafiri na baadhi ya wakati wanaweza kuzidisha hata muda wa masaa mawili na abiria kupata hasara kwa kuharibu utaratibu mzima.

(a) Je, ni haki zipi wanapaswa kupatiwa abiria pindi ikitokea usumbufu huo wakati wao wanapochelewa dakika chache hawawezi kuruhusiwa kusafiri na pesa za tiketi hazirejeshwi.

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya kadhia ya Shirika ambalo limewasabishia hasara bila ya kuwafidia abiria hao.

54. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga barabara za ndani kwa kiwango cha lami ili kuepusha kujazwa kifusi barabara hizo kila mwaka. Na kwa kuwa barabara inayotoka Kilima juu na Tundangaa hujaa maji kila mvua zinaponyesha na kupelekea shughuli za uwekezaji zinazofanywa kupitia barabara hiyo kukwama.

Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili kuwezesha shughuli za uwekezaji kuimarika zaidi.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

126. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Katika malengo yake ya Bajeti ya mwaka 2021/2022, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ni kuimarisha ukulima wa zao la mwani kwa kutafuta masoko yenye tija ambapo kwa mwaka huu wa bajeti Shirika linatarajia kununua jumla ya tani 1000 za mwani kwa gharama ya Tshs. 920.0 milioni pamoja na kuratibu na kuanzisha kiwanda cha kusarifu mwani.

(a) Je, Wizara mpaka sasa imeshanunua tani ngapi za mwani.

(b) Je, Shirika mpaka sasa limefikia hatua gani katika malengo yake.

## III. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (P.A.C):**

Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (P.A.C) ya Mwaka 2017/2018 na 2019/2020.

**Mjumbe wa Kamati ya Wabunge watano wanaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Ripoti ya Wabunge watano wanaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Zanzibar,**
**28 Februari, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**